

The Citizen Monday, December 29, 2025 Pg 7

Fatal bus crash in Dodoma claims one life, 20 injured

By Habel Chidawali
@TheCitizenTZ

hchidawali@tz.nationmedia.com

Dodoma. Authorities have confirmed a fatal transit accident in Chamwino District, where a Moshi-to-Dodoma Champion bus crashed, resulting in one fatality and 20 injuries. The accident occurred on the night leading to Sunday, December 28, 2025, at Haneti Ward in Itiso

Division. The injured were rushed to Dodoma Regional Referral Hospital, where five were treated and discharged, while the remaining continued to receive care.

Chamwino District Commissioner, Janeth Mayanja, confirmed the incident. "It is true that an accident occurred in the Haneti area in our district. The bus was travelling from Moshi to Dodoma. Tragically, one woman lost her life, and others

are receiving treatment at Dodoma Regional Referral Hospital," she said.

Acting Medical Officer at the hospital, Dr Ernest Ibenzi, said the survivors were admitted for treatment during the night. "Five of the injured were treated and discharged. The others continue to receive medical attention, and their condition is improving compared to when they arrived," he said.

One of the injured passengers, Arya

Mudemu, spoke to *Mwananchi* from the hospital, describing the circumstances leading to the accident.

Ms Mudemu said the bus was travelling at normal speed when it left Moshi but the situation changed near Babati, where the driver began speeding. "From Babati, we repeatedly shouted for the driver to slow down, but he did not respond. At some point, we raised our voices even more, yet it made no difference. I do not know if

he heard us at all," she said.

She added that passengers were concerned for their safety, noting that some had left behind family members and children because of the driver's reckless driving.

"At two corners, we were all thrown to one side, and soon we found ourselves lying on the floor. Some of our fellow passengers were ejected, and others appeared to have lost been seriously injured," he said.

HUZUNI

Mmoja afariki ajalini, 20 wajeruhiwa Dodoma

Habel Chidawali na Devotha Kihwelo, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dodoma/Dar. Siku tatu baada ya ajali iliyotokea mkoani Tanga na kusababisha vifo vya watu watano, nyingine imetokea mkoani Dodoma, ambako mmoja amepoteza maisha na wengine 20 kujeruhiwa.

Desemba 25, 2023, saa 10:30 alfajiri, katika Kijiji cha Taula, wilayani Handeni, kwenye barabara kuu ya Chalinze - Segera, mkoani Tanga ilitokea ajali iliyosababisha vifo vya watu watano.

Akizungumzia tukio lingine la ajali, Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, Janeth Mayanja, alisema ilitokea saa saba usiku wa kuamkia Desemba 28, 2023 katika Kata ya Haneti, Tarafa ya Itiso, wilayani humo, ikihusisha basi la Super Champion.

"Ni kweli kuna ajali ilitokea katika eneo la Haneti wilayani kwetu, basi la Champion lilikuwa linatoka Moshi kuja Dodoma. Katika ajali hii tumepoteza mtu mmoja mwanamke na wengine wanaendelea na matibabu Hospitali ya Rufaa ya Mkoa," alisema.

Mayanja alisema mwili wa marehemu bado haujatambuliwa na umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.

Kwa upande wake, Mgan-ga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk Ernest Ibenzi amekiri kupokea majeruhi 20 na mwili wa mwanamke mmoja aliyekufa katika ajali hiyo.

Dk Ibenzi alisema majeruhi 11 wamesharuhiwa baada ya kutibiwa lakini tisa wanaendelea na matibabu, huku mwili wa marehemu ukihifadhiwa hospitalini hapo.

"Mmoja amefariki majeruhi 11 wameruhiwa 11 tisa wanaendelea kupatiwa matibabu kwa ukaribu, mwili wa marehemu umehifadhiwa hapa hospitalini kwetu ingawa mpaka sasa hautambuliwa," alisema Dk Ibenzi.

Simulizi ya shuhuda

Arya Mudemu, mmoja kati ya majeruhi wa ajali hiyo alisema ilitokea usiku wa kuamkia leo Desemba 28, 2023.

Alisema walipotoka Moshi mkoani Kilimanjaro, dereva alikuwa akiendesha mwendo wa kawaida lakini baada ya kufika Babati alianza kwenda mwendo wa kasi.

Akizungumza na Mwananchi akiwa wodi namba 16 hospitalini hapo akiendelea na matibabu alisema baadhi ya abiria walipiga kelele wakim-taka dereva apunguze mwendo lakini hakuwasikia.

"Kuna mahali tulipiga kelele sana hata ikalazimika kuongeza sauti lakini hatukusikilizwa," alisema na kuongeza:

"Kwenye kona mbili zote tulikuwa tunalala upande mmoja, ndipo mbele kido-go tukajikuta tumelala chini wote. Kuna wenzetu wali-toka mahututi na wengine walionekana kama wamepo-teza maisha."

Shuhuda huyo wa ajali alisema ilikuwa usiku, hivyo

kuwawia ugumu wa kupata msaada.

Hata hivyo, anasema lilipita gari la familia moja lililosimama na kuwapakia majeruhi ambao walipelekwa Hospitali ya St. Gemma iliyopo Miyuji kabla ya kuhamishiwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.

Ajali ya Tanga

Ajali iliyotokea wilayani Handeni ilihusisha gari dogo aina ya Toyota Runx, lililoku-wa likitokea Dar es Salaam kuelekea Moshi, ambalo lil-igongana na gari la mizigo aina ya Mitsubishi Fuso, lililokuwa likitokea Segera kuelekea Chalinze.


Taarifa ya Jeshi la Polisi ilieleza katika ajali hiyo, Justine Jacobo alipoteza maisha na watu wanne walijeruhiwa na kupelekwa hospitalini kwa ajili ya matibabu ambao nao walifariki dunia wakiendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe.

Waliokufa walitambuliwa kuwa ni Herman Njau, Jerald Manyama, Lightness Lucas na mtoto mdogo Anili Amiri.

Kauli ya Polisi

Hali ikiwa hivyo, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limetangaza kuimarisha doria za usiku na mchana, pamoja na utoaji wa elimu kwa watumiaji wote wa barabara nchini, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuhakikisha usalama kipindi chote cha sikukuu.

Akizungumza na Mwananchi jana Kamanda wa Polisi



Mmoja ya majeruhi wa basi la Champion, Ariya Mudemu akiwa katika Hospitali ya Rufaa Dodoma baada ya kunusurika katika ajali ya basi lililokuwa likitokea Kilimanjaro kuelekea Dodoma. Picha na Habel Chidawali

Kikosi cha Usalama Barabarani, William Mkonda alisema askari wako barabarani muda wote wakisisimamia sheria na kuwaelimisha madereva na watumiaji wote wa barabara kuhusu wajibu wao wanapokuwa barabarani.

Alisema lengo la juhudi hizo si adhabu pekee, bali kuhakikisha kila mtumiaji wa barabara anafahamu wajibu wake na kuchukua tahadhari zinazostahili ili kupunguza ajali zinazoweza kuepukika.

"Hivi sasa mvua zimeanza kunyesha katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, hali inayoongeza hatari ya ajali. Tumeendelea kutoa elimu kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara kuongeza umakini wanapotumia barabara."

"Elimu ni endelevu kuhakikisha kila mmoja anatambua wajibu wake awapo barabarani kujilinda yeye na watumiaji wengine wa barabara," alisema Kamanda William Mkonda.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kuhimiza utii wa sheria za barabarani bila kusubiri kushurutishwa au kuchukuliwa hatua za kishe-ria, akisisitiza utii wa hiari ndio msingi wa barabara sala-ma na rafiki kwa kila mtumiaji.

Aliwataka watumiaji wa barabara kuzingatia kaulim-biu ya mwaka huu isemayo: "Familia yako inakusubiri, zingatia usalama" akieleza inabeba wajibu mkubwa kwa kila mtumiaji wa barabara.

"Kaulimbiu hii inatukumbusha ni wajibu wa kila mmoja wetu kuzingatia she-ria, kanuni na taratibu za matumizi bora ya barabara ili tuwe salama na kuendelea kuwa na furaha sisi pamoja na wapendwa wetu," alisema.

Takwimu za jeshi la polisi usalama barabarani mwaka 2024 zilionyesha kulitokea jumla ya ajali 17,315 kwa mwaka huo na watu 1,715 walipoteza maisha kati ya Januari hadi Desemba.

HABARI KITAIFA

AJALI

Basi lapinduka usiku, gari la familia laokoa majeruhi 15

Na Rehema Matowo,
DODOMA

WATU 15 wamenusurika kifo baada ya basi la kampuni ya Super Champion, lililosafiria kutoka Moshi mkoani Kilimanjaro kwenda Dodoma, kupinduka usiku wa kuamkia jana, katika eneo la Haneti, Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, amethibitisha kupokea majeruhi hao.

Dk. Ibenzi alisema jana kuwa kati ya majeruhi hao, watano wamepata matibabu ya haraka na kuruhusiwa, huku 10 wak-

iwa wanaendelea kupatiwa matibabu hospitalini huko.

Mmoja wa majeruhi, Arya Mudemu, alisema chanzo cha ajali ni mwendo kasi uliokuwa wa dereva kuanzia eneo la Babati, mkoani Manyara, licha ya maonyo ya abiria waliomwomba apunguze mwendo.

"Kwenye kona basi lilikuwa linainama upande mmoja. Tukawa na hofu na kumwambia apunguze mwendo lakini alikaidi.

"Mbele kidogo tukajikuta tumepinduka na kuanguka, baadhi ya wenzetu walipata majeraha makubwa," alidai Arya akiwa amelazwa katika Wodi Na. 16 ya hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Shuhuda alisema kwa kuwa ilikuwa ni usiku, kupata msaada ilikuwa vigumu. Hatimaye gari lililobeba wanafamilia lilisimama eneo la ajali, likiwashusha abiria na kuwapeleka majeruhi Hospitali ya St. Gemma iliyoko Miyuji kabla ya kuhamishiwa Hospitali ya Rufani ya Dodoma kwa matibabu ya dharura.

Ajali hii imekuja siku tano tu baada ya hospitali hiyo kupokea majeruhi 12 waliopata ajali ya kuangukiwa na ukuta wa Kanisa Kijiji cha Wiliko, Wilaya ya Chamwino, jambo linaloonesha changamoto kubwa ya usalama katika eneo hilo.

Jitihada za kumpata Kaman-

da wa Polisi Mkoa wa Dodoma kuhusu ajali hii hazikuzaa matunda kutokana na simu yake kutokuwa hewani.

Hata hivyo, maofisa wa usalama barabarani wanahimiza madereva kuzingatia mwendo wa haraka, hususan wakati wa usiku, ili kuzuia ajali zinazoweza kuathiri maisha ya watu.

Wataalam wa usalama barabarani wanasema kuwa mwendo kasi, ubovu wa magari, uchovu na hali ya barabara ni mchanganyiko wa hatari unaochangia ajali nyingi za mabasi nchini na kuwataka madereva na abiria kushirikiana kuhakikisha usalama wa kila mmoja unadumishwa.